BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 27 Septemba, 2022
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2021/2022.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

113. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kuanza kutumika kwa mfumo wa ZanMalipo kulileta matumaini katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali yakiwemo mapato ya Halmashauri na Mabaraza ya Miji. Hata hivyo, ufanisi wa ZanMalipo ni wa mashaka.

Je, ni upi utaratibu wa sasa wa kukusanya mapato ya Halmashauri na Mabaraza ya Miji ya Unguja na Pemba.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

100. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Pamoja na jitihada za Serikali zinazohitaji pongezi kwa kujaribu kulitatua kwa ujumla wake suala la malipo ya ushuru wa ongezeko la thamani (Value Added Tax) kwa bidhaa zitokazo au zipitazo Tanzania Bara, inasikitisha kwamba bado kuna kudharauliwa kukubwa kwa taratibu walizokubaliana Serikali mbili, ya SMZ na SMT, kwa kuwalipisha wafanyabiashara na wananchi wengine malipo ya VAT sehemu zaidi ya moja na wala sio tu kufidia kodi iliyopungua. Hii inasababisha mlaji wa kawaida kugharamia bidhaa ambazo zina kodi tatu za VAT, kwa mfano (i) VAT inayolipwa katika Bandari ya Dar es Salaam kwa bidhaa A, (ii) VAT inayolipwa katika Bandari ya Zanzibar kwa bidhaa hiyo hiyo A, (iii) VAT inayolipwa dukani Zanzibar kwa muuzaji wa jumla kwa bidhaa hiyo hiyo A, na (iv) VAT inayolipwa na mlaji kwa muuzaji wa reja reja kwa bidhaa hiyo hiyo A.

(a) Je, ni yepi maelezo sahihi ya Serikali kwa jambo hili.

(b) Je, ni hatua gani wananchi wanaweza kuzichukua iwapo watalazimishwa kulipa VAT zaidi ya moja.

105. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) zote ni Taasisi za SMZ. Na kwa kuwa Taasisi hizi zimekuwa zikisaidiana katika mikakati ya kibiashara kwa miaka mingi sasa. Na kwa kuwa kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na mabadiliko ya kibiashara kati ya Taasisi mbili hizi.

(a) Je, ni upi mpango mpya wa kimkakati kibiashara wa Taasisi hizi.

(b) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuziimarisha Taasisi hizi kibiashara Bara na Visiwani.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

48. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na tabia ya baadhi ya Kampuni za Usafiri wa Anga zinazomiliki ndege ndogo za usafirishaji wa abiria baina ya Unguja na Pemba pamoja na Dar es Salaam, kutumia rubani mmoja kwa kusafirisha abiria, pamoja na ndege zao hizo kuwa ni viti vya rubani pamoja na msaidizi wake. Hali hii ni hatari kwa abiria pale rubani huyo anapopatwa na tatizo la kiafya.

(a) Je, kwa nini Serikali haijalishughulikia tatizo hili kwa muda mrefu sasa.

(b) Je, Serikali baada ya kuikumbusha tatizo hili, itachukua hatua gani kuliondosha.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

69. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wananchi wengi wanaoishi maeneo ya ukanda wa bahari hasa Pemba wamekuwa wakiunda vikundi mbali mbali vya uhifadhi wa mazingira ikiwemo uhifadhi wa mikoko. Kwa bahati mbaya baadhi ya watendaji wa Wizara yako wamekuwa wakiwavunja moyo wanavikundi hao kwa kisingizio cha kutovitambua vikundi hivyo.

(a) Je, hadi sasa, Serikali inavitambua vikundi vingapi vya uhifadhi wa mikoko na kwa utaratibu upi.

(b) Je, hadi sasa, ni msaada gani na kwa utaratibu upi vimepatiwa vikundi hivyo.

117. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Eneo la Kizingo kuanzia Maisara mpaka maeneo ya Mazizini Unguja, limekuwa maarufu kwa watu mbali mbali kufanya mazoezi karibu na fukwe. Hata hivyo, baadhi ya watu wanapeleka wanyama kama ng'ombe na mbwa kwenda kuwakogesha katika maji ya fukwe za bahari katika eneo hilo, huku watu wengine wakiendelea na mazoezi yao ya viungo.

(a) Je, Wizara yako imejiridhisha kama kufanya hivyo

hakuleti madhara ya kiafya na kimazingira.

(b) Je, kuchanganyika kwa wanyama wanaokoshwa na watu kuogolea pamoja, hakuondoi haiba ya fukwe katika eneo hilo.

(c) Je, kuna miongozo yoyote iliyowekwa ya kudhibiti wanyama kuingizwa kwenye fukwe za bahari, hasa katika eneo hilo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

91. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Imefahamika kwamba viwanja vya michezo vya Malindi vitabadilishwa matumizi yake ya asili kama ilivyo kwenye utaratibu wa Mipango Miji ya Zanzibar. Jambo hili limewasikitisha sana wananchi walio wengi wa Zanzibar.

Je, ni upi utakuwa mbadala wa viwanja vya michezo vya Malindi na lini sehemu mbadala itaanza kutumika.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

142. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa sote tunafahamu kuwa umeme ni nishati muhimu kwa maendeleo ya mwanadamu. Na kwa kuwa katika jimbo la Nungwi, wananchi walio wengi kwa zaidi ya miezi mitatu sasa, wamejisajili katika Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) na kupatiwa "RISITI" za malipo na wanaendelea kusubiri bila ya kupatiwa huduma hii ndani ya makaazi yao.

(a) Je, mteja akishatimiza sharti la kulipia laki mbili za kitanzania, kuna sharti jengine lolote linalomzuia kupatiwa huduma ya umeme.

(b) Je, Shirika halioni kuwa linawavunja moyo wateja wake na kuwakosesha imani kwa Shirika lao.

(c) Je, Wizara yako inawataka wananchi wanaokosa huduma ya umeme baada ya kuilipia wakimbilie wapi.

<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

71. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Ulimwengu umekuwa ukilizungumzia sana na kulipa kipaumbele suala zima la sayansi, teknolojia na ubunifu pamoja na ukweli kwamba, katika nchi yetu suala hili limekuwa la kinadharia zaidi kuliko uhalisia.

(a) Je, Serikali yetu ya Zanzibar inalichukuliaje jambo hili kiutekelezaji.

(b) Je, kwa kiasi gani vyuo vyetu vinaihusisha mitaala yao na masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

126. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Baadhi ya vitabu vya lugha ya Kiengereza vya skuli za msingi vimebainika na dosari za kukosekana mada (Topics) za vitenzi (Tenses) ambazo ni mada mama katika kuwafunza watoto lugha ya kiengereza.

(a) Je, Wizara ya Elimu imeshagundua dosari hiyo.

(b) Je, hatua gani zimechukuliwa kurekebisha dosari hizo.

(c) Je, Wizara inawashirikisha vipi walimu wa lugha ya Kiengereza wa skuli za msingi wakati wa kutunga vitabu hivyo.

## III. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2021/2022.

Zanzibar,
27 Septemba, 2022.

(Raya Issa Msellem)
<u>KATIBU WA BARAZA</u>.